MAMLAKA YA HALI YA HEWA
TANZANIA

# JARIDA LA HALI YA HEWA


**Na: 01 Msimu wa kilimo 2017/18 Tathmini ya Kipindi cha Oktoba 1-10, 2017 na matazamio kwa kipindi cha Oktoba 11-20, 2017**

**MUHTASARI**

- Maeneo yanayopata misimu miwili ya mvua, wakulima wanaendelea kuandaa mashamba na kupanda mazao.
- Mazao katika baadhi ya maeneo ya mkoa wa Kagera yalikuwa katika hatua ya palizi husussan wilaya ya Bukoba.
- Kutokana na hali ya ukavu inayoendelea hususan maeneo yanayopata msimu mmoja wa mvua na nyanda za juu kaskazini mashariki, wafugaji wanashauriwa kuchukua hatua stahiki kutokana na upungufu wa maji na malisho.

## MIFUMO YA HALI YA HEWA KATIKA KIPINDI CHA OKTOBA 1-10, 2017

Katika kipindi tajwa, migandamizo ya hewa iliyo kusini mwa dunia (St. Helena na Mascarene) iliendelea kupungua nguvu na hivyo kudhoofisha mkondo wa mgandamizo wa hewa wa Afrika Mashariki. Migandamizo iliyo kaskazini mwa dunia (Azores na Siberia) nayo pia iliendelea kuimarika, hivyo kuruhusu ukanda wa mvua (ITCZ) kushuka kuelekea kusini mwa dunia. Joto la juu kidogo ya wastani liliendelea katika eneo la kusini-magharibi mwa Bahari ya Hindi. Kwa upande mwingine joto la bahari lilikuwa juu ya wastani katika maeneo ya kusini-mashariki mwa Bahari ya Atlantiki (karibu na pwani ya Angola) na kusababisha hali ya vipindi vichache vya mvua katika maeneo ya magharibi mwa nchi na yale yaliyopo katika ukanda wa ziwa Viktoria.




**Kielelezo**. Mwenendo wa mvua katika kipindi cha Oktoba 1 - 10,

## MWENENDO WA MVUA KATIKA KIPINDI CHA OKTOBA 1-10, 2017

Kutokana na mifumo ya hali ya hewa, mvua kati ya milimita (mm) 26 na 150 zilinyesha katika maeneo ya kanda ya ziwa Viktoria, magharibi na nyanda za juu kaskazini magharibi (hususan maeneo ya miinuko) na mvua za milimita zaidi 150 zilinyesha katika baadhi ya sehemu ya ziwa Victoria. Kama inavyoonekana katika Kielelezo.

## TATHMINI YA HALI YA KILIMO KATIKA KIPINDI CHA OKTOBA 1-10, 2017

Wakulima katika maeneo mengi yanayopata mvua za vuli waliendelea na uandaaji wa mashamba isipokuwa katika mkoa wa Kagera hususan wilaya ya Bukoba ambapo wameanza kupalilia mazao. Kwa maeneo yanayopata msimu mmoja wa mvua wakulima wanaendelea na maandalizi kwa ajili ya msimu unaotarajiwa kuanza mwezi Novemba na Disemba. Upatikanaji wa maji na malisho kwa mifugo ulikuwa wa wastani katika maeneo mengi ya nchi, isipokuwa katika baadhi ya maeneo ya mikoa ya Mwanza, Mara, Simiyu, Shinyanga, Singida, Arusha, Manyara na

Dodoma ambako hali ya maji na malisho iliendelea kupungua kuliko maeneo mengine nchini.

## HALI YA MAJI ILIVYOKUWA KATIKA KIPINDI CHA OKTOBA 1-10, 2017

Kina cha maji katika mabwawa na mtiririko wa maji katika mito viliendelea kupungua katika maeneo mengi ya nchi kutokana na hali ya ukavu inayoendelea.

## MIFUMO YA HALI YA HEWA INAVYOTARAJIWA KATIKA KIPINDI CHA OKTOBA 11-20, 2017

Migandamizo ya hewa iliyo kusini mwa dunia inatarajiwa kuendelea kupungua nguvu. Wakati, ile migandamizo iliyopo sehemu za kaskazini mwa dunia inatarajiwa kuendelea kuimarika na hivyo kuruhusu ukanda wa mvua wa ITCZ kuendelea kushuka kuelekea sehemu ya kusini mwa dunia. Joto la bahari la juu kidogo ya wastani linatarajiwa katika eneo la kusini-magharibi mwa Bahari ya Hindi na hii inatarajiwa kuendelea kusababisha upepo wenye unyevunyevu kiasi kuvuma kutoka kusini na kusini-mashariki kuelekea katika ukanda wa Pwani na kuleta mvua katika ukanda huo. Kwa upande mwingine joto la bahari la juu ya wastani linatarajiwa kusini-mashariki mwa Bahari ya Atlantiki; hii inatarajiwa kusababisha hali ya ukavu katika maeneo ya Magharibi mwa nchi pamoja na ukanda wa ziwa Victoria.

## HALI YA HEWA INAVYOTARAJIWA KATIKA KIPINDI CHA OKTOBA 11-20, 2017

Kutokana na mifumo ya hali ya hewa, maeneo mengi yanatarajiwa kuwa . Maeneo ya **ukanda ya ziwa Viktoria (Mikoa ya Kagera, Geita, Shinyanga, Mwanza, Mara na Simiyu)** yanatarajiwa kupata vipindi vya mvua zitakazoambatana na ngurumo. Maeneo ya **nyanda za juu kaskazini mashariki (Mikoa ya Kilimanjaro, Arusha na Manyara)** yanatarajiwa kuwa makavu kwa ujumla na vipindi vichache vya mvua hususan katika maeneo ya miinuko. Maeneo ya **Pwani ya kaskazini (Mikoa ya Tanga, Pwani, Dar es Salaam, Morogoro pamoja na visiwa vya Unguja na Pemba)** yanatarajiwa kupata vipindi vichache vya mvua , hususani kuelekea mwishoni mwa kipindi hiki. Maeneo ya **Magharibi mwa nchi (Mikoa ya Kigoma, Katavi na Tabora)** yanatarajiwa kupata vipindi vichache vya mvua vikiambatana na ngurumo**.** Maeneo ya **kanda ya kusini (Mkoa wa Ruvuma na kasikazini mwa mkoa wa Morogoro)** yanatarajiwa kuwa na hali ya ukavu na baridi. Maeneo ya **Kanda ya kati (Mikoa ya Dodoma na Singida)** yanatarajiwa kuwa makavu. Maeneo ya **Pwani ya kusini (Mikoa ya Mtwara na Lindi)** yanatarajiwa kuwa makavu na vipindi vichache vya mvua. Maeneo ya **nyanda za juu kusini magharibi (Mikoa ya Rukwa, Songwe, Njombe, Iringa na Mbeya)** yanatarajiwa kuwa na hali ya ukavu kwa ujumla, vipindi vichache vya mvua hususani katika maeneo ya miinuko.

## MATARAJIO NA USHAURI KATIKA KIPINDI CHA OKTOBA 11-20, 2017

Mvua zinatarajiwa kuongezeka kwa maeneo yanayopata misimu miwili ya mvua hususan pwani ya kaskazini na kanda ya ziwa Viktoria. Wakulima wa maeneo haya wanashauriwa kuzitumia mvua hizi kupanda. Hata hivyo wakulima wa maeneo ya Kagera na pwani ya kaskazini wanashauriwa kupanda mazao yanayostahimili ukame kutokana na mvua za wastani hadi chini ya wastani zinazotarajiwa. Kwa maeneo yanayopata msimu mmoja wa mvua pamoja na nyanda za juu kaskazini mashariki, mvua katika kipindi hiki hazitarajiwi kutosheleza uoteshaji wa mazao ya msimu. Wafugaji wanashauriwa kuchukua hatua stahiki kwa kuzingatia ushauri wa maafisa ugani katika maeneo yao.

## HALI YA MAJI INAVYOTARAJIWA KATIKA KIPINDI CHA OKTOBA 11-20, 2017

Kina cha maji katika mabwawa na utiririkaji wa mito inatarajiwa kuongezeko kidogo katika maeneo yanayopata mvua mara mbili kwa mwaka hususan bonde la maji la ziwa viktori. Watumiaji wa maji wanashauriwa kuyatumia kwa uangalifu.

*Jarida limetayarishwa na:*

Mamlaka ya Hali ya Hewa Tanzania
Ghorofa ya 3 -Ubungo Plaza – Barabara ya Morogoro, Dar es Salaam-Jamhuri ya Muungano wa Tanzania